# HOTUBA YA WAZIRI WA KILIMO NA USHIRIKA MHESHIMIWA WILLIAM KUSILA (MB): WAKATI AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2000/2001

## I. UTANGULIZI

1. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa likae kama Kamati ya Matumizi ili liweze kujadili na kuidhinisha makadirio ya matumizi ya Wizara ya Kilimo na Ushirika kwa kipindi cha mwaka wa fedha wa 2000/2001.

2. Mheshimiwa Spika, kabla ya kutoa maelezo juu ya hali ya kilimo, mifugo na maendeleo ya ushirika nchini, naomba nitumie nafasi hii kutoa salamu za rambi rambi kwa Mheshimiwa Rais, Familia ya marehemu na Watanzania wote kwa kifo cha Baba wa Taifa **Mwalimu Julius Kambarage Nyerere,** kilichotokea tarehe 14 Oktoba 1999. Wizara yangu itamkumbuka daima Mwalimu kama mpenda amani, mtetezi wa wanyonge, hasa wakulima na wafugaji wa Tanzania, na jinsi alivyokuwa karibu nao siku zote za uhai wake. Tunamkumbuka alivyoheshimu shughuli za kilimo katika kuinua hali ya maisha ya wakulima na wafugaji. Tunamkumbuka pia kwa kuitisha semina na mikutano mbalimbali na kusisitiza umuhimu wa kilimo katika maendeleo ya nchi. Kampeni aliyoanzisha ya "SIASA NI KILIMO" ni mfano tosha kuelezea jinsi Mwalimu alivyokipa umuhimu kilimo. Wizara yangu itaendeleza jitihada za Mwalimu J.K. Nyerere katika kuendeleza kilimo na ufugaji nchini. Mwenyezi Mungu aiweke roho ya Mwalimu Nyerere mahali pema peponi.

3. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 1999/2000 Taifa pia liliwapoteza Wabunge wafuatao: Marehemu Stanley Kinuno, aliyekuwa Mbunge wa Nyang'hwale, Marehemu Salum Ngajulage, aliyekuwa Mbunge wa Liwale na Marehemu Kanali Yusuf Ramia, aliyekuwa Mbunge wa Bagamoyo. Kwa niaba ya Wizara yangu na mimi mwenyewe, natoa pole kwa familia za Marehemu na Mwenyezi Mungu aziweke roho zao mahali pema peponi, Amina.

4. Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais, Benjamin William Mkapa, kwa jitihada zake za kuinua hali ya kilimo nchini. Katika mwaka 1999/2000 Mheshimiwa Rais aliitisha na kuendesha Mikutano ya aina yake ambayo iliwakutanisha viongozi wa ngazi mbalimbali nchini huko Dar es Salaam na Mwanza ili kujadili na kuzungumzia mipango mbalimbali itakayosaidia kuleta mapinduzi ya kilimo, mifugo na ushirika nchini. Mikutano hii chini ya uenyekiti wake,

ilihudhuriwa na Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Mawaziri, Wakuu wa Mikoa, baadhi ya Makatibu Wakuu, Wakuu wa Mashirika ya Umma, wataalam kutoka sekta mbalimbali za Umma na Binafsi na Viongozi wengine wa Kitaifa. Wizara yangu inaendelea kutekeleza maamuzi ya Mikutano hiyo.

5. Mheshimiwa Spika, vile vile namshukuru Waziri Mkuu, Mheshimiwa Frederick, Tluway Sumaye (Mb), kwa kuunda Kamati mwezi Septemba 1999, iliyochambua matatizo yanayoikabili sekta ya kilimo na mifugo na kuishauri Serikali hatua za kuchukua ili kuendeleza sekta hii. Wizara yangu inaendelea kutekeleza mapendekezo ya kamati hii.

6. Mheshimiwa Spika, naomba kukupongeza wewe binafsi kwa kuchaguliwa kwako kuwa Mwenyekiti wa Sekretariati ya Mabunge ya Jumuiya ya Madola. Kuchaguliwa kwako kumelijengea Bunge hili na Taifa kwa ujumla heshima kubwa sana. Kwa niaba ya Wizara ya Kilimo na Ushirika, na kwa niaba yangu, tunakutakia kila la kheri katika wadhifa wako huo. Naomba kuchukua nafasi hii vile vile kuwapongeza Wabunge wapya waliojiunga na Bunge lako Tukufu, ambao ni Mhe. Hasnain Mohamed Murji, Mbunge wa Mitema, Mhe. John Kibaso, Mbunge wa Temeke, Mhe. Venance Ngula, Mbunge wa Ubungo, Mhe. James Msalika, Mbunge wa Nyang'hwale na Mhe. Azim Premji, Mbunge wa Kigoma Mjini. Pongezi nyingi pia nazitoa kwa Waheshimiwa Wabunge walioweza kurudi tena katika Bunge lako Tukufu baada ya kushinda uchaguzi katika majimbo yao, ambao ni Mhe. Ibrahim Msabaha, Mbunge wa Kibaha, Mhe. Sebastian Kinyondo, Mbunge wa Bukoba Vijijini na Mhe. William Shija, Mbunge wa Sengerema.

7. Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii vile vile, kumpongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Frederick Tluway Sumaye (Mb) kwa hotuba yake nzuri ambayo imefafanua masuala mengi ya kilimo, mifugo na ushirika. Aidha, nawapongeza Mawaziri wenzangu walionitangulia kwa hotuba zao ambazo zimefafanua masuala mengi ya kiuchumi na kijamii. Vile vile, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge, hususan Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi inayoongozwa na Mbunge wa Tunduru, Mhe. Juma Jamaldine Akukweti, kwa michango yao ambayo imesaidia kuonyesha maeneo ya kuzingatia katika utekelezaji wa mpango wa Wizara yangu kwa mwaka 2000/2001

**Hali ya Chakula Duniani**

8. Mheshimiwa Spika, taarifa ya mwezi Aprili, 2000 ya Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO), inaeleza kwamba makisio ya awali ya uzalishaji wa nafaka duniani katika kipindi cha 1999/2000 unatazamiwa

kufikia tani milioni 1,890 kiasi ambacho ni ongezeko la asilimia moja ikilinganishwa na tani milioni 1,850 za mwaka 1998/99. Kiasi kitakachopatikana hakitaweza kutosheleza mahitaji ya chakula kwa mwaka 2000/2001, na hivyo kusababisha akiba ya nafaka iliyopo sasa kutumiwa na kupungua. Inakadiriwa kuwa nchi 34 duniani zinahitaji chakula cha msaada. Kati ya hizo, nchi 15 ziko Afrika, Kusini mwa jangwa la Sahara.

9. Mheshimiwa Spika, katika Bara la Afrika inaonyesha kuwa kutakuwa na upungufu mkubwa wa chakula katika kipindi cha 2000/2001 hasa katika nchi zilizoko mashariki mwa Afrika, hususan Ethiopia, Eritrea, Djibout, Somalia, Sudan na Kenya. Hali hii imesababishwa na ukame mkubwa uliolikumba eneo hili na kusababisha baa la njaa ambalo limeathiri watu wapatao milioni 16 wanaohitaji msaada wa dharura wa chakula. Mafuriko yaliyozikumba nchi za kusini mwa Afrika mwanzoni mwa mwaka huu yameathiri kwa kiasi kikubwa matazamio ya upatikanaji wa chakula ijapokuwa hali ya chakula inatazamiwa kuwa ya wastani katika nchi za Botswana, Malawi, Afrika ya Kusini, Zambia na Zimbabwe. Msumbiji ndiyo iliathirika sana na mafuriko haya na watu milioni 1.9 waliathiriwa vibaya. Mheshimiwa Spika, nafurahi kulitangazia Bunge lako Tukufu kwamba Serikali ya Tanzania ilitoa msaada wa dharura wa jumla ya tani 1,000 za mahindi kwa Serikali ya Msumbiji ili kuwasaidia wananchi wake walioathiriwa na mafuriko hayo.

10. Mheshimiwa Spika, katika nchi za Maziwa Makuu za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Rwanda na Burundi hali ya chakula si ya kuridhisha kutokana na vita. Hali kadhalika vita vya wenyewe kwa wenyewe nchini Angola bado vinaendelea na kuathiri vibaya uzalishaji wa chakula. Zaidi ya watu milioni moja wanakabiliwa na upungufu wa chakula nchini humo. Tofauti na nchi za Mashariki na Kusini mwa Afrika nchi za Ukanda wa Sahel za Afrika ya Magharibi hususan Burkina Fasso, Cape Verde, Gambia, Mali, Mauritiania na Senegal zinatazamiwa kuwa na mavuno ya kuridhisha. Kwa ujumla, katika Bara la Afrika inaonyesha kuwa kutakuwa na upungufu wa chakula ambao utasababisha ongezeko la mahitaji ya chakula cha msaada na cha kununua.

## II. MAPITIO YA MWAKA 1999/2000

### Mazao ya Chakula.

11. Mheshimiwa Spika, Mahitaji ya chakula kwa mwaka 1999/2000 yalikadiriwa kuwa tani milioni 6.84. Kati ya hizo, mahitaji ya mazao ya nafaka yalikuwa tani milioni 4.35 na yasiyo nafaka yalikuwa tani milioni

2.49. Hivyo, kwa mazao ya nafaka kulikuwa na upungufu wa jumla ya tani 558,500 ambao hata hivyo umefidiwa na mazao yasiyokuwa ya nafaka (Tazama Jedwali ….).

12. Mheshimiwa Spika, baadhi ya mikoa nchini, ikiwa ni pamoja na Morogoro, Lindi, Dodoma, Mbeya, Singida, Arusha, Mara, Mwanza, Tabora, Shinyanga, Kagera, Iringa na Kilimanjaro iliathirika na milipuko ya wanyama, wadudu na ndege waharibifu wa mimea ambao walipunguza mavuno. Kwa ujumla, uzalishaji wa mazao ya nafaka na yasiyo ya nafaka ulipungua ukilinganisha na malengo kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na:-

a) Mvua za vuli kunyesha chini ya viwango vya kawaida,

b) Kuchelewa kuanza kwa mvua za masika ambazo zilinyesha kwa mtawanyiko mbaya na kukatikakatika kwa vipindi virefu kwa baadhi ya mikoa.

c) Upungufu wa mbegu bora kwa wakulima ambao ulipunguza viwango vya uzalishaji na maeneo yaliyolimwa.

d) Matumizi madogo ya pembejeo hasa mbolea kutokana na uwezo mdogo wa wakulima kununua pembejeo hizo.

e) Athari kutokana na milipuko ya wadudu, wanyama na ndege waharibifu.

13. Mheshimiwa Spika, takwimu za awali za uzalishaji wa mazao ya chakula nchini kwa msimu wa 1999/2000 na mahitaji kwa kipindi cha 2000/2001 unaonyesha kuwa uzalishaji wa mazao ya chakula utafikia tani milioni 6.68 ambapo tani milioni 3.55 ni za mazao ya nafaka na tani milioni 3.13 ni za mazao yasiyo nafaka. Makisio ya mahitaji ya chakula ni tani milioni 7.36. Uzalishaji huu utakidhi mahitaji ya chakula kwa asilimia 91. Kwa hiyo kutakuwepo na upungufu wa chakula nchini wa tani 681,000 (Tazama Jedwali ……). Kwa upande wa uzalishaji wa mazao ya nafaka, ambayo hutumiwa na wananchi wengi kwa chakula, mikoa inayoonyesha kujitosheleza kwa mazao hayo ni pamoja na Iringa,Tanga, Tabora, Mbeya, Rukwa na Ruvuma. Mikoa itakayojitosheleza kwa chakula kutokana na ziada ya mazao yasiyo nafaka ni Kagera, Kigoma, Lindi na Mtwara. Mikoa inayotegemewa kuwa na upungufu wa chakula ni Dodoma, Arusha, Morogoro, Singida, Kilimanjaro, Mwanza, Shinyanga, Pwani na Mara. Hata hivyo, hali halisi itajulikana baada ya zoezi la kutathmini hali ya chakula linaloendelea mikoani kukamilika mwishoni mwa mwezi Julai 2000.

14. Mheshimiwa Spika, hali ya upatikanaji wa chakula kwa kipindi cha mwaka 2000/2001 itategemea viwango vya uzalishaji chakula msimu huu, akiba waliyojiwekea wakulima, akiba ya wafanyabiashara na hifadhi ya Chakula ya Taifa (SGR) ambayo mpaka sasa ipo katika viwango vya kuridhisha. Hivi sasa maghala ya hifadhi ya chakula ya Taifa yanazo karibu tani 80,000 za chakula kwa ajili ya dharura.

**Mazao ya Biashara**

15. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 1999/2000 uzalishaji wa mazao ya biashara ulikuwa na ongezeko kwa mazao ya korosho, chai, pareto, kahawa na sukari ukilinganisha na uzalishaji wa 1998/99. Uzalishaji wa korosho uliongezeka kwa asilimia 18 kutoka tani 110,000 hadi tani 130,000, chai kwa asilimia 14.2 kutoka tani 21,704 hadi tani 24,792, pareto kwa asilimia 100 kutoka tani 500 hadi 1,000, kahawa kwa asilimia 29.4 kutoka tani 37,092 hadi tani 48,000 na sukari kwa asilimia 5.3 kutoka tani 111,040 hadi tani 116,933. Uzalishaji wa mazao ya tumbaku, pamba na mkonge ulipungua kutokana na matatizo ya upatikanaji wa pembejeo, mbegu, ukame ulioendelea kwa muda mrefu katika maeneo yanayozalisha mazao hayo na bei ndogo katika soko la dunia. Uzalishaji wa tumbaku ulipungua kwa asilimia 39.7 kutoka tani 44,264 hadi tani 26,670, pamba kwa asilimia 4.3 kutoka marobota 201, 400 hadi marobota 192,730 na mkonge kwa asilimia 12.4 kutoka tani 23,228 hadi tani 20,359 (Tazama jedwali…).

**Mazao yasiyo Asili**

16. Mheshimiwa Spika, katika msimu wa 1999/2000, mazao ya mbegu za mafuta kama ufuta, mawese, nyonyo na soya yaliendelea kupata msukumo wa uzalishaji na utafiti. Vile vile, uzalishaji wa mazao ya mboga, matunda, maua na viungo umeendelea kukua na kupata masoko ndani na nje ya nchi. Kwa mfano, mwaka 1998 kiasi cha tani 6,706 za mboga, maua tani 2,000, viungo tani 1,241 na matunda tani 3,888 ziliuzwa nchi za nje na kulileteа Taifa kiasi cha shilingi bilioni 10.3. Wizara yangu, katika kuendeleza mazao haya, imeanzisha mpango wa kuzalisha miche bora kwa kutumia wakulima wazalishaji wa vitalu ambao huzalisha na kusambaza mbegu kwa wakulima. Mashirika yasiyokuwa ya kiserikali nayo yamehusika katika kutoa mafunzo ya kilimo bora cha mboga, matunda na maua. Mafunzo juu ya usindikaji wa mboga na matunda yaliendelea kutolewa na taasisi mbalimbali nchini.

**Mazao yatokanayo na Mifugo**

17. Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa mifugo na mazao yake umeendelea kukua katika kipindi cha 1999/2000, licha ya kuwepo kwa uhaba wa mvua na milipuko ya magonjwa mbalimbali ya mifugo nchini. Baadhi ya maeneo hayakupata mvua za kutosha na hivyo kuathiri upatikanaji wa maji na malisho kwa mifugo. Ufugaji wa ng'ombe wa maziwa hasa katika mikoa ya Kagera, Tanga, Iringa, Mbeya, Kilimanjaro na Arusha umeendelea kuwa na mafanikio kutokana na Programu ya Uendelezaji wa Ng'ombe wa Maziwa.

18. Mheshimiwa Spika, Uzalishaji wa nyama uliongezeka kutoka tani 268,000 mwaka 1998/99 na kufikia tani 301,000 (asilimia 12.3). Uzalishaji wa maziwa uliongezeka kutoka lita milioni 687 hadi lita milioni 710 (asilimia 3). Uzalishaji wa mayai ya kuku uliongezeka kutoka mayai milioni 430 hadi milioni 450 (asilimia 4.7). Ukusanyaji wa ngozi nao uliongezeka kutoka ngozi 2,350,000 na kufikia ngozi 2,421,000 (asilimia 3). Hata hivyo, uuzaji wa ngozi nchi za nje ulishuka kwa asilimia 17 kutoka ngozi 1,825,000 mwaka 1998/99 na kufikia ngozi 1,516,000 mwaka 1999/2000. Sababu kubwa ya kushuka kwa uuzaji ngozi nchi za nje kunatokana na kushuka kwa bei ya ngozi katika masoko ya bara la Asia kulikosababishwa na kuyumba kwa uchumi katika nchi hizo. (Tazama Jedwali …..).

**Huduma za Ushauri wa Kitaalam wa Kilimo na Ufugaji**

19. Mheshimiwa Spika, kupitia miradi ya Southern Highlands Extension and Rural Financial Services (SHERFS) unaofadhiliwa na IFAD, National Agricultural Extension Project unaofadhiliwa na Benki ya Dunia, na Programu ya Uendelezaji Ng'ombe wa maziwa, Wataalamu waliendelea kutoa ushauri kuhusu masuala ya kilimo na ufugaji bora. Miradi hii inasaidia katika upatikanaji wa vitendea kazi, vifaa vya usafiri pamoja na kugharamia mafunzo kwa wakulima na wataalam. Inakadiriwa kuwa Wakulima na wafugaji wapatao milioni 2.12 waliweza kufikiwa na kupewa ushauri. Aidha, njia nyingine kama radio, magazeti na vipeperushi vilitumika.

20. Mheshimiwa Spika, Chama cha Wakulima – Tanzania Agricultural Society (TASO) kwa kushirikiana na Muungano wa Vyama vya Ushirika (TFC) walisimamia Maonyesho ya Wakulima Kitaifa yaliyofanyika Mkoani Arusha mara tano mfululizo. Napenda kuwashukuru viongozi na wananchi wote wa mikoa ya Arusha na Kilimanjaro kwa kazi nzuri waliyoifanya.

Maonyesho hayo pia yalifanyika katika ngazi mbalimbali katika mikoa. Mwaka huu maonyesho hayo yatafanyika kitaifa Morogoro. Napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza viongozi wa Mkoa wa Morogoro kwa kukubali kuandaa maonyesho hayo. Umuhimu wa maonyesho haya ni katika kuwaelimisha wakulima na wafugaji kuhusu kilimo na ufugaji bora.

**Kilimo cha Umwagiliaji**

21. Mheshimiwa Spika, Wizara iliendelea kusimamia ujenzi na ukarabati wa miradi midogo midogo ya umwagiliaji ya wakulima vijijini. Katika mwaka 1999/2000 jumla ya hekta 2,000 zilianza kutumika chini ya mradi wa Madibira unaopata mkopo kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB). Mradi wa kuendeleza wakulima wadogo katika mabonde ya Mto Rufiji na Pangani unaofadhiliwa na Benki ya Dunia unakusudia kuendeleza jumla ya hekta 9,000. Programu husishi ya uendelezaji wa wakulima mdogo katika mikoa ya ukame (Participatory Irrigation Development Programme) ya Dodoma, Singida, Tabora, Shinyanga, Mwanza na Arusha utaendeleza hekta 11,400. Aidha, jumla ya hekta 8,000 zinaendelezwa katika mikoa ya Mbeya, Iringa na Morogoro chini ya mradi wa Agriculture Sector Support Program unaopata msaada kutoka Serikali ya Denmark.

**Utafiti wa Kilimo na Mifugo**

22. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 1999/2000, utafiti wa kilimo na mifugo uliendelea kutekelezwa chini ya mradi wa Tanzania Agricultural Research Project – TARP II. Kipaumbele kimewekwa katika programu za utafiti zinazoshughulikia matatizo ya wakulima wadogo hasa wakulima wanawake. Utafiti wa mazao kutafuta aina za mbegu bora za mazao mbalimbali ya nafaka (mahindi, ngano, mpunga, mtama), mboga, matunda, mbaazi na viazi mviringo umeimarishwa. Aidha, mbinu za kuhifadhi mazao kabla na baada ya kuvunwa, udhibiti wa magugu sugu pamoja na magonjwa mbalimbali uliendelea kufanyiwa uchunguzi. Katika kipindi cha mwaka 1999/2000 vituo mbalimbali vya utafiti vilikamilisha utafiti na kutoa aina bora ya mbegu ya mtama iitwayo "*Macia*" na mbegu ya mbaazi iitwayo "*komboa*", ambazo zinastawi vizuri na kutoa mazao mengi kuliko mbegu za kawaida tunazotumia.

23. Mheshimiwa Spika, katika juhudi za kupunguza vifo vya kuku vijijini vinavyotokana na ugonjwa wa kideri, utafiti ulifanikiwa kutathmini

chanjo ya kideri isiyohitaji jokofu. Majaribio yalifanyika katika Kanda ya Kusini na Mashariki katika wilaya za Mtwara, Masasi na Handeni. Matokeo ya awali yanaonyesha matumaini mazuri. Hivyo chanjo hiyo itazalishwa kwa wingi na maabara za Kanda (VICs) kwa majaribio yatakayoenezwa sehemu kubwa ya nchi. Vile vile utafiti wa lishe, malisho na uzalishaji wa mifugo umeendelea kwa kuandaa mikakati mipya kwa kila kanda ya utafiti ili kujua aina ya malisho ya miti jamii ya mikunde inayofaa kwa mifugo.

24. Mheshimiwa Spika, Sekta binafsi imeendelea kushirikishwa na kuchangia gharama za utafiti kwa mazao ya pamba, kahawa, chai, tumbaku, miwa, shayiri na korosho. Utafiti wa zao la chai tayari umebinafsishwa kwa kuanzisha taasisi inayosimamia utafiti wa zao hilo, “**Tea Research Institute of Tanzania” (TRIT)**. Uanzishaji wa Taasisi za Usimamizi wa utafiti wa kahawa **“Tanzania Coffee Research Institute” (TACRI)** na tumbaku **“Tobacco Research Institute of Tanzania” (TORITA)** upo katika hatua za mwisho.

25. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Benki ya Dunia imeanzisha Mfuko wa Utafiti wa Kilimo Kitaifa **“National Agricultural Research Funds” – (NARF)** na Kikanda “**Zonal Agricultural Research Fund” (ZARF).** Madhumuni ya kuanzisha mifuko hii ni kuweza kuhamasisha na kushirikisha matumizi ya raslimali zilizopo kitaifa na kikanda. Programu za utafiti zinazotokana na msukumo wa wakulima wenyewe **“Client Oriented Research” (COR)** katika Kanda ya Ziwa imesaidia sana kuhamasisha kupata fedha za utafiti kutoka katika mashirika ambayo siyo ya Kiserikali. Kanda ya Kaskazini nayo imeanzisha Programu ya “Client Oriented Research” ambapo utafiti utafanyika kwa mikataba. Kanda za utafiti za Kati, Kusini na Ziwa zimefanya majadiliano na Uongozi wa Halmashauri ili ziweze kuchangia utafiti. Majadiliano kati ya Wizara na Halmashauri katika Kanda zilizobaki yanaendelea ili nazo ziweze kuchangia katika mazao ya chakula na mifugo. Hatua hii inakusudiwa kuzipa Halmashauri sauti zaidi katika kupanga maeneo ya kipaumbele ya Utafiti kwenye sehemu zao.

**Mafunzo ya Kilimo na Mifugo**

26. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 1999/2000, Wizara yangu iliendeleza shughuli za mafunzo katika hali ngumu ya fedha. Mchango wa Serikali katika kugharamia shughuli mbalimbali za mafunzo umekuwa ukipungua mwaka hadi mwaka hivyo kuathiri kwa kiasi kikubwa shughuli na ubora wa mafunzo yatolewayo. Kiwango cha ada kinacholipwa na wanafunzi hakiwezi kukidhi gharama zote. Hali halisi inaonyesha kuwa

viwango hivyo viko juu ya uwezo wa wanaohitaji mafunzo hayo. Mchango wa Serikali bado ni muhimu sana katika kuweka mazingira bora ili kuvutia wanafunzi wengi zaidi kujiunga na vyuo hivi. Katika kipindi cha 1999/2000, Wizara yangu kwa kushirikiana na wafadhili iliweza kutoa mafunzo ya aina mbalimbali juu ya mbinu bora za kilimo na ufugaji kwa wanafunzi 286 . Aidha, wakulima na wafugaji 1,268 walipata mafunzo ya muda mfupi vyuoni.

**Upatikanaji wa Pembejeo na Zana za Kilimo**

27. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 1999/2000 Wizara yangu iliendelea kuweka msukumo wa kuwahamasisha na kuwashirikisha wakala wa pembejeo na wanunuzi wa mazao ya biashara ili waendelee kuagiza na kusambaza pembejeo kwa wakulima. Makadirio ya mahitaji ya aina mbali mbali za mbolea kwa msimu wa 1999/2000 yalikuwa tani 170,000. Upatikanaji ulikuwa jumla ya tani 130,240, ambazo kati ya hizo albaki ya mwaka wa 1998/1999 ni tani 78,740 na kiasi kilichobaki tani 51,500 kiliagizwa kutoka nje ya nchi. Kiasi cha mbolea kilichopatikana ni asilimia 76.6 ya makadirio ya mahitaji. Makadirio ya mahitaji ya madawa ya mimea kwa msimu wa 1999/2000 yalikuwa lita 3,200,000 za madawa ya maji na tani 9,000 za madawa ya unga. Upatikanaji wa madawa ulikuwa lita 696,072 (asilimia 21.8) na tani 8,129.2 (asilimia 90). Matumizi ya madawa yamepungua sana kutokana na bei kubwa za madawa na uwezo mdogo kifedha wa wakulima na wafugaji.

28. Mheshimiwa Spika, makadirio ya mahitaji ya mbegu bora kwa nchi nzima ni tani 30,000. Upatikanaji wa mbegu bora zilizothibitishwa msimu wa 1999/2000 zilifikia jumla ya tani 5,695 kwa mazao ya nafaka, mikunde na mbegu za mafuta. Hali hii ni ongezeko la asilimia 20 ikilinganishwa na msimu uliopita wa 1998/99. Aidha, mashamba ya mbegu ya Taifa, wakulima binafsi na mashirika yasiyokuwa ya kiserikali (NGOs) yanayoshughulikia na uzalishaji wa mbegu yamechangia jumla ya tani 1,142. Baadhi ya makampuni ambayo hayazalishi mbegu hapa nchini yaliweza kuagiza kutoka nje jumla ya tani 1,090. Kati ya mbegu zilizopatikana mwaka 1999/2000, tani 505 zilizalishwa kutoka kwenye mashamba ya Taifa. Wakala wa Serikali TOSCA waliendelea kudhibiti ubora wa mbegu.

29. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 1999/2000 upatikanaji wa zana bora za kilimo umeendelea kuwa chini ya mahitaji. Jitihada zilizofanyika katika msimu wa 1999/2000 ni pamoja na kuongeza matumizi ya aina mbalimbali ya zana. Jumla ya matrekta madogo 30 yaliingizwa nchini kwa msaada wa

Japan (20) na Jamhuri ya Korea (10). Aidha matrekta 50 makubwa yaliingizwa nchini. Wizara ikishirikiana na Halmashauri iliendelea kuhimiza matumizi ya zana za kukokotwa na wanyama. Pamoja na zana nyingine ndogo ndogo kama vile majembe ya mkono, pampu za kunyunyizia dawa.

30. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 1999/2000, mchango wa mfuko wa Pembejeo za Kilimo (Agricultural Input Trust Fund) katika kusaidia upatikanaji wa pembejeo umekuwa sio wa kuridhisha. Hii inatokana na mfuko kutoweza kukusanya mikopo ambayo imetolewa kwa wakala wa pembejeo na baadhi ya wakulima. Hadi Machi 2000, Mfuko ulikuwa umetoa mikopo 259 yenye thamani ya shilingi bilioni 5.8 kwa mawakala wa pembejeo na wakulima na kati hizo ni shilingi bilioni 1.54 tu zilizorejeshwa. Wizara yangu imesimamisha kutoa mikopo zaidi hadi hapo hali ya ukusanyaji wa madeni utakapokuwa mzuri ili tuweze kuendelea kutoa mikopo mingine. Mfuko umeandaa mkakati wa kuongeza kasi ya ukusanyaji wa mikopo, ikiwa ni pamoja na kuwatumia Wakala wa kukusanya madeni (Debt Collectors). Wadaiwa sugu wenye madeni makubwa wamekabidhiwa kwa wakusanya madeni, ikiwa ni pamoja na taarifa za kuuzwa kwa dhamana zao. Wale watakaoshindwa kurejesha mikopo watachukuliwa hatua za kisheria.

**Udhibiti wa Magonjwa, Wadudu, Ndege na Wanyama Waharibifu wa Mimea na Mifugo**

31. Mheshimiwa Spika, milipuko ya ndege aina ya *Quelea quelea* imeendelea kuathiri sehemu mbalimbali nchini. Katika kukabiliana na tatizo hili, Wizara yangu imefanya shughuli za udhibiti katika mikoa ya Arusha, Dodoma, Kilimanjaro, Mara, Mbeya, Morogoro, Mwanza, Singida, Shinyanga na Tabora. Katika msimu wa 1999/2000 jumla ya makundi 137 yanayokisiwa kuwa na ndege milioni 97.3 yalidhibitiwa katika eneo la hekta 2,731 pamoja na mazalio 28 ya ndege ambayo yalionekana katika mikoa hiyo na shughuli za udhibiti zinaendelea.

32. Mheshimiwa Spika, tatizo la nzige wekundu limeendelea kujitokeza katika sehemu mbalimbali nchini. Hata hivyo Wizara yangu kwa kushirikiana na **International Red Locust Control Organisation for Central and Southern Africa** (**IRLCO – CSA)** imefanikiwa kudhibiti milipuko ya nzige hawa kwa ufanisi. Wizara tayari imekwisha fanya savei na imeonekana kuwa nzige wengi watazaliana katika maeneo ya mabonde ya Iku/Katavi, Malagarasi na Wembere Kaskazini.

33 Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Aprili 2000, sehemu kadhaa za mikoa ya Kilimanjaro, Iringa na Arusha zilikuwa zimeshambuliwa na viwavi jeshi.

Wizara yangu ilisambaza madawa ya kudhibiti wadudu hawa katika mikoa ambayo milipuko ilitabiriwa kutokea. Hadi kufikia mwezi Aprili 2000 kiasi cha lita 12,000 za madawa zilikuwa zimesambazwa.

34. Mheshimiwa Spika, udhibiti husishi (Integrated Pest Management) umeendelea kuwa njia muhimu ya kudhibiti wadudu na magonjwa ya mimea na mazao. Wadudu maadui (bio-control agents) walizalishwa na kusambazwa katika maeneo yaliyoathiriwa na utitiri na kidung'ata wa muhogo, dumuzi, inzi wa machungwa, gugu maji na panzi wa muhogo. Aidha, mbegu zinazostahimili magonjwa na wadudu wa muhogo ziliagizwa kutoka Uganda na kuzalishwa hapa nchini. Uchunguzi wa mbegu hizi dhidi ya magonjwa na wadudu unaendelea na wakulima wataanza kugawiwa mbegu mara tu uchunguzi huu utakapokamilika.

35. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 1999/2000 mlipuko wa panya uliendelea kuikumba mikoa ya Lindi, Tanga na Morogoro. Katika baadhi ya maeneo yaliyoathirika, wakulima walipoteza kiasi kikubwa cha mbegu zilizopandwa mashambani na mazao yaliyokuwa yamehifadhiwa kwa ajili ya chakula hasa mahindi na muhogo. Katika kukabiliana na tatizo hili Wizara yangu ilipeleka sumu ya panya kwenye Halmashauri za Lindi na Ulanga ili kudhibiti milipuko hiyo. Aidha, Wizara iliendesha mafunzo ya mbinu za kupambana na panya kwa wataalam 30 kutoka katika wilaya zote za mkoa wa Lindi.

36. Mheshimiwa Spika, magonjwa ya milipuko ya mifugo kama vile ugonjwa wa homa ya mapafu, miguu na midogo, chambavu, kimeta na kichaa cha mbwa yamejitokeza katika sehemu mbalimbali nchini. Magonjwa yaenezwayo na kupe pamoja na mbung'o yameenea katika baadhi ya maeneo. Hata hivyo, magonjwa ya sotoka na Homa ya Bonde la Ufa yametokomezwa nchini. Kukosekana kwa huduma za maji ya kutosha na maeneo maalum kwa ajili ya ufugaji vimesababisha wafugaji wengi kuhama hama na mifugo yao na hivyo kuongeza usambazaji wa magojwa mbalimbali ya mifugo hasa Homa ya Mapafu. Tayari wilaya 42 zimeathirika katika mikoa ya Mbeya, Iringa, Dodoma, Rukwa, Tabora, Arusha, Shinyanga, Kagera, Morogoro, Tanga, Pwani na Mtwara.

37. Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na milipuko ya magonjwa ya mifugo na athari zake kwa wafugaji hatua kadhaa zimechukuliwa. Hatua hizi ni pamoja na kuchanja ng'ombe milioni 1.8, kuzuia kuenea kwa ugonjwa wa homa ya mapafu, mbwa 60,000 walichanjwa kuzuia kichaa cha mbwa, kuzalisha dozi 500,000 za dawa ya chanjo ya kuzuia ugonjwa wa mdondo, chanjo ya kukinga ng'ombe dhidi ya ugonjwa wa Ndigana kali (ECF) yalifanyika.

Sampuli 4,700 zilifanyiwa uchunguzi ili kuhakiki kuwapo au kutokuwapo kwa ugonjwa wa sotoka. Mipango ya kuanzisha utekelezaji wa mradi wa kuondoa ndorobo katika mikoa ya Kagera na Tanga bado inaendelea.

**Maendeleo ya Ushirika**

38. Mheshimiwa Spika, hali ya Vyama vya Ushirika nchini bado haijawa nzuri. Vyama vingi vya Ushirika vinafanya kazi ya uwakala wa makampuni binafsi na sehemu kubwa ya vyama hivi viliendelea kuwa sinzia (dormant) ambapo kati ya Vyama Vikuu 48 ni Vyama Vikuu 16 tu vilivyoweza kujikongoja na kutoa huduma kwa wanachama wake. Vyama hivyo ni ACU (Arusha), KNCU (Kilimanjaro), UCU (Usambara), TDCU (Tanga), SAMCU (Songea), LATCU (Mpanda), WETCU (Tabora), SHIRECU (Shinyanga), NCU (Nyanza), KCU (Kagera), KDCU (Karagwe), TACU (Tarime), ISAYULA (Mbozi), MBOCU (Mbozi), BCU (Biharamulo) na SCCULT (Savings and Credit Cooperative League of Tanzania).

39. Mheshimiwa Spika, jukumu la ufungaji wa vitabu vya hesabu za Vyama vya Ushirika ni wa Halmashauri na watendaji wakuu wa Vyama vya Ushirika. Taarifa zinaonyesha kuwa hali ya ufungaji na ukaguzi wa vitabu vya hesabu bado hairidhishi. (Jedwali….). Vyama vingine vya ushirika vimeshindwa kukaguliwa kwa wakati kutokana na uongozi mbaya. Viongozi wa vyama hivyo wameshindwa kukamilisha ufungaji wa hesabu na kuondolewa madarakani. Aidha baadhi ya vyama vimeshindwa kulipia ada ya ukaguzi kutokana na vyama hivyo kuwa dhaifu kifedha.

40. Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na matatizo yanayovikabili Vyama vya Ushirika nchini, suala la elimu kwa wanaushirika limepewa kipaumbele. Mafunzo ambayo yamekuwa yakitolewa yanajumuisha kozi kuhusu kazi za uandishi wa Vyama vya Ushirika, utunzaji wa vitabu vya hesabu, kazi za Halmashauri na kusoma mizania. Katika kipindi cha 1999/2000, Chuo cha Ushirika Moshi kimewapatia mafunzo mbalimbali ya uhasibu na uongozi jumla ya Halmashauri 271, wanachama 3,000 na watendaji wa vyama 394. Masomo haya hutolewa kwa njia ya Posta na Chuo cha Ushirika Moshi. Aidha, Wizara yangu inachapisha nakala za Sera ya Ushirika ambazo zitasambazwa kwenye Vyama vya Ushirika ikiwa ni pamoja na kutoa mafunzo juu ya sera hiyo kwa kushirikiana na Chuo cha Ushirika na Shirikisho la Vyama vya Ushirika nchini. Mafunzo haya yatatolewa kwa njia ya redio, machapisho mbalimbali na Semina. Vile vile, mwongozo wa uendeshaji wa Vyama vya Ushirika unaandaliwa.

41. Mheshimiwa Spika, pamoja na matatizo mengi ambayo yamekuwa

yakivikabili Vyama vya Ushirika, idadi ya vyama hivyo imeongezeka kutoka vyama 4,500 mwaka 1995 hadi kufikia vyama 4,821 mwaka 2000. Idadi ya Vyama vya Akiba na Mikopo (SACCOS) vimeongezeka kutoka 728 mwaka 1998 na kufikia 902 mwaka 2000 vikiwa na hisa zenye thamani ya shilingi bilioni 4.4 na amana za thamani ya shilingi bilioni 6.91. Hata hivyo, idadi ya wanachama katika Vyama vya Ushirika bado ni ndogo. Vyama hivi vina wanachama 603,659 ambao ni asilimia 12 ya wakulima.

42. Mheshimiwa Spika, Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo (SACCOS) vimepewa msukumo ili viwe kitovu cha uchumi katika maeneo ya vijijini na mijini. Vyama hivi vina nafasi ya kuwakomboa wakulima na wafanyakazi kutokana na hali duni ya maisha. SACCOS zinatumiwa na vyama vya mazao kama Benki na zinaweza kuungana pamoja na vyama vya aina nyingine kuunda Benki ya Ushirika kwa ajili ya kukabiliana na mahitaji ya mikopo. Mfano mzuri ni Benki ya Ushirika ya mkoa wa Kilimanjaro ambayo mpaka sasa ina maendeleo mazuri.

43. Mheshimiwa Spika, kufuatia mkutano wa Ushirika wa Rais na viongozi mbalimbali kuhusu maendeleo ya Ushirika uliofanyika Mwanza, mwishoni mwa mwezi Machi 2000, Mheshimiwa Rais aliteua tume tatu zitakazohusika na zoezi zima la kufufua Ushirika nchini. Tume ya kwanza inahusika na kutoa ushauri kwa Rais kuhusu kufufua, kurekebisha na kuimarisha Vyama vya Ushirika nchini. Tume ya pili ni ya kufuatilia kesi mbalimbali za Vyama vya Ushirika. Tume ya tatu inahusika na jinsi gani Vyama Vikuu vya Ushirika mkoani Kagera visiweze kufilisiwa na mabenki. Ripoti za tume hizi bado zinasubiriwa ili hatua zinazostahili ziweze kuchukuliwa.

44. Mheshimiwa Spika, uwajibikaji wa viongozi katika Vyama vya Ushirika umekuwa ni kikwazo na chanzo cha ubadhirifu na wizi. Ili kudhibiti hali hii Wizara kwa kushirikiana na Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali imefanya ukaguzi maalum kwa Shirikisho la Vyama vya Ushirika nchini (TFC) na taarifa hiyo imesomwa kwenye Mkutano Mkuu Maalum ulioitishwa na Mrajis tarehe 26/5/2000 ambapo Viongozi Wakuu watatu wa Shirikisho walisimamishwa kazi.

**Marekebisho ya Mashirika ya Umma**

45. Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha mwaka 1999/2000 mashirika yafuatayo yalirekebishwa kwa nia ya kubinafsishwa:

(a) Kampuni ya sukari TPC-Moshi

(b) Mali za NMC: Maghala 18, vinu vya mpunga na mahindi vya Mwanza na NMC makao makuu.

(c) Shamba la Kahe-NAFCO.
(d) Mamlaka ya Chai: Viwanda vya chai Lushoto na Rungwe.

Aidha, majadiliano yanafanyika kati ya Tume ya Rais ya Kurebisha Mashirika ya Umma (PSRC) na wawekezaji kwa ajili ya mali zifuatazo:

(i) Kampuni ya Chai Mufindi
(ii) Shamba la chai Malangali
(iii) Mashamba ya Chai Maruku.
(iv) TTA Tawi la Dabaga

**Maendeleo ya Watumishi**

46. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 1999/2000, Wizara yangu iliendelea na kazi ya kuwaondolea watumishi kero zinazohusiana na utumishi wao. Kazi ya kukusanya na kuchambua kumbukumbu za watumishi kwa ajili ya kuandaa zoezi la kuwapandisha vyeo watumishi hao iliendelea. Baada ya kukamilisha utayarishaji wa tange kwa kada zote, mapendekezo ya kuwapandisha vyeo kwa msererreko watumishi wapatao 7,243 kutoka Idara zote za Wizara yamekwisha pelekwa Idara Kuu ya Utumishi kwa ajili ya kupata kibali cha Mamlaka husika. Tayari watumishi 316 wamekwisha pandishwa vyeo mpaka mwishoni mwa mwezi Mei 2000. Kazi hiyo inaendelea

47. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 1999/2000, Wizara yangu imekamilisha zoezi la kuhamishia watumishi wa Wizara ya Kilimo na Ushirika kwenye Sekretariat za Mikoa na Serikali za Mitaa. Kati ya watumishi 12,172, watumishi 4,266 wamebaki chini ya Wizara na wengine 7,906 wamehamishiwa kwenye Halmashauri za Wilaya. Zoezi la kuwapanga upya katika Halmashauri linaendelea. Waliobaki Wizarani wako Makao Makuu, Vituo vya: Utafiti, Udhibiti Magonjwa, Wadudu na Ndege Waharibifu, Ukaguzi wa Mazao Mipakani na Vyuo (Tazama Jendwali …….).

**Matumizi ya Fedha za Mpango na Bajeti ya Mwaka 1999/2000**

48. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 1999/2000 Wizara ya Kilimo na Ushirika ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi milioni 44,420.00 kwa ajili ya kutekeleza mpango. Jumla ya shilingi milioni 15,720.20 kwa matumizi ya kawaida na shilingi milioni 28,700.70 kwa shughuli za miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo za maendeleo shilingi milioni 2,437.50 ni fedha za hapa na shilingi milioni 26,263.20 ni fedha za kigeni. Hadi Mei, 2000 matumizi ya kawaida yalikuwa shilingi milioni 6,723.00 (asilimia 43). Matumizi ya

fedha za miradi ya maendeleo yalikuwa shilingi milioni 80.00 fedha za hapa (asilimia 3.3) zilizotengwa. Fedha za kigeni zimetumika jumla ya shilingi milioni 13,806.00 ambazo ni asilimia 53 tu ya fedha zilizotengwa. Kushindwa kutumia fedha za kigeni zilizotengwa kutokana na kukosekana kwa fedha za hapa (Counterpart Funds).

## III MPANGO WA MAENDELEO WA MWAKA 2000/2001

49. Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo ya utekelezaji wa mpango wa mwaka 1999/2000, ambayo yamedhihirisha upungufu mkubwa wa fedha za maendeleo uliojitokeza na kusababisha utekelezaji kuwa mdogo kulingana na malengo imetulazimu kuingiza shughuli nyingi za 1999/2000 kwenye mpango wa mwaka 2000/2001. Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2000/2001 umeandaliwa kwa kuzingatia mabadiliko ya sera za kijumla za uchumi na za sekta, mwongozo uliotolewa na Tume ya Mipango pamoja na Hazina kuhusu utayarishaji wa Mpango wa Muda wa Kati na Mfumo wa Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2000/2001 – 2002/2003 "(Medium Term Expenditure Framework MTEF)", Sera za Kilimo, Mifugo na Ushirika pamoja na muundo na Majukumu ya Wizara ya Kilimo na Ushirika.

### Huduma za Ushauri kwa Wakulima na Wafugaji

50. Mheshimiwa Spika, mwaka 1997, Serikali ilifanya mabadiliko ya muundo wa utendaji kazi katika ngazi za Mikoa na Halmashauri. Mabadiliko haya yalifanywa kwa nia ya kuboresha na kuongeza ufanisi katika utoaji huduma kwa wananchi kwa kupeleka utaalam na rasilimali karibu zaidi na pia kuweza kujua vema matakwa na vipaumbele vya wananchi. Kuanzishwa kwa mfumo huo mpya, kumeleta mabadiliko katika majukumu na wajibu wa Wizara yangu katika kusimamia na kutoa huduma za kilimo, mifogo na ushirika nchini. Kulingana na Sera ya Kilimo na Mifugo huduma za ushauri zimeainishwa kama uhawilishaji wa teknolojia kutoka kwa wataalam kwenda kwa wakulima na wafugaji. Wataalam hawa ni kiungo kati ya wakulima na wafugaji na Taasisi za utafiti mahali ambapo teknolojia za kilimo zinaendelezwa, kujaribiwa na kurekebishwa ili kuongeza tija katika kilimo na ufugaji. Kutokana na uamuzi wa Serikali wa kupeleka shughuli za utekelezaji wa ushauri wa kilimo na ufugaji kwenye Serikali za Mitaa, majukumu ya Wizara ya Kilimo na Ushirika kwa ujumla yanahusu; sera na ushauri wa kitaalam. (Tazama Jedwali).

51. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu itaendelea kushirikiana na Serikali za Mitaa ili kuhakikisha kuwa wataalamu wanaendelea kuwashauri wakulima na wafugaji kuhusu kuongeza uzalishaji na tija katika uzalishaji. Wizara

itaendelea kugharamia nyenzo za kazi kwa kupitia miradi iliyopo. Nyumba 32 za mabwana shamba zitakamilishwa kujengwa katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini. Mafunzo kwa wakulima na wataalam pia yataendelea kutolewa.

52 Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inaandaa mradi wa kuimarisha rutuba ya udongo "Soil Fertility Recapitalization and Agricultural Intensification Project" (SOFRAIP) unaolenga katika kuongeza tija na uzalishaji, kupima na kurutubisha udongo, kueneza taaluma kwa wakulima na wafugaji, mafunzo kwa wasambazaji wa pembejeo, kuendeleza vyama vya akiba na mikopo, kutoa mikopo kwa wakulima na wafugaji na upatikanaji wa pembejeo.

**Utafiti wa Kilimo na Mifugo**

53. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2000/2001, Wizara yangu itaendelea kuratibu na kufanya utafiti wa kilimo na mifugo nchini kwa kuzingatia sera ya kilimo na mifugo pamoja na mifumo ya kilimo na ufugaji kulingana na mahitaji ya Kanda zenyewe. Sambamba na sera hiyo, mikakati ambayo itatumika, kuendeleza utafiti wa kilimo na mifugo ni kama ifuatavyo:

- Kuhusisha zaidi sekta binafsi na Halmashauri katika kupanga na kugharamia utafiti.

- Kuimarisha uhusiano wa Mfumo wa Taifa wa Utafiti wa Kilimo na Mifugo **(National Agricultural Research System)** na mifumo ya taasisi nyingine kwenye Kanda na pia Taasisi nyingine zilizoko nje ya nchi.

- Kuendeleza utafiti wa kilimo na mifugo kwa kuzingatia hali halisi ya wakulima vijijini, masuala ya jinsia na utunzaji wa mazingira.

- Kuendelea kuwapa watafiti mafunzo ya muda mfupi na mrefu ili kuongeza ufanisi wao wa kazi pamoja na motisha.

- Kuimarisha huduma za kusambaza matokeo ya utafiti kwa kushirikiana na mabwana shamba pamoja na wakulima.

**Mafunzo ya Kilimo na Mifugo**

54. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2000/2001, Wizara yangu inategemea kufanya yafuatayo katika kuendeleza mafunzo ya kilimo na mifugo:

- Kuendelea kutoa mafunzo kwa Mabwana Shamba.

- Kutoa mafunzo kwa wakulima na wafugaji 2,600 ili kuwapa uwezo mkubwa wa uzalishaji.

- Kuweka mazingira mazuri ya mafunzo vyuoni kwa kukarabati na kuimarisha vifaa vya mafunzo kwa vitendo.

- Kurekebisha mitaala ya kozi nne (4) za stashahada na kutayarisha vitabu viwili vya kiada na vitabu viwili vya kiongozi cha mwalimu.

**Udhibiti wa Magonjwa, Wadudu na Ndege waharibifu wa Mimea na Mifugo**

55. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2000/2001 huduma za udhibiti wa magonjwa, wadudu na ndege waharibifu wa mazao na mifugo zitaendelea kuimarishwa, hasa katika maeneo yafuatayo:

§ Kuimarisha na kupanua teknolojia ya udhibiti husishi ili ienee kutoka mikoa tatu ilivyo sasa, hadi mikoa tisa ( Shinyanga, Arusha, Kagera, Mara, Tabora, Tanga, Morogoro, Mwanza na Kilimanjaro).

§ Kuendelea kutoa mafunzo kwa wakulima, wafugaji na wafanyakazi kuhusu matumizi sahihi ya madawa.

§ Kuimarisha ushirikiano kati ya Serikali, Vyama visivyokuwa vya Kiserikali (NGOs) na watafiti wanaojihusisha na utumiaji wa madawa ya asili kwa ajili ya kudhibiti wadudu waharibifu wa mimea na mifugo.

§ Kuhakikisha kuwa mitego yote ya kunasia nondo inafanya kazi.

§ Kuimarisha njia za mawasiliano ili taarifa za uchunguzi wa milipuko ya magonjwa, wanyama, wadudu na ndege waharibifu ziweze kupatikana mapema na kufanyiwa kazi.

§ Kufanya savei ya kutathmini mafanikio ya ueneaji wa wadudu (bioagents) wanaosambazwa.

§ Kujenga vituo 5 vya kuzalisha wadudu wa kudhibiti gugu maji.

56. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu itaendelea kuimarisha shughuli za

kudhibiti milipuko ya magonjwa ya mifugo kama vile ya miguu na midomo, homa ya mapafu, chambavu, kimeta, kichaa cha mbwa na ndigana. Aidha Wizara yangu itaendelea kufanya majaribio ya kukinga ng'ombe dhidi ya ugonjwa wa ndigana kali (ECF) na kuzalisha dawa ya chanjo ya kuzuia ugonjwa wa mdondo kwenye kituo cha Utafiti wa Mifugo cha Temeke, Dar es Salaam.

**Kilimo cha Umwagiliaji**

57. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2000/2001, Wizara yangu itahusika na uendelezaji wa miradi iliyopewa kipaumbele katika kuendeleza kilimo cha umwagiliaji. Aidha, Wizara itaendelea na utekelezaji wa miradi inayopata fedha za msaada kutoka serikali ya Denmark chini ya Programu ya kusaidia sekta ya kilimo kuendeleza kilimo cha umwagiliaji kwa wakulima wadogo wadogo katika mikoa ya Iringa, Mbeya na Morogoro; Programmu ya kuendeleza kilimo cha umwagiliaji katika mikoa ya ukame ya Dodoma, Singida, Tabora, Shinyanga, Mwanza na Arusha, pamoja na mradi wa kuendeleza wakulima wadogo wadogo katika mabonde ya mto Rufiji na Pangani. Vile vile, Wizara yangu itaendelea na juhudi za kukamilisha taratibu za kufanikisha utekelezaji wa miradi ifuatayo:-

§ Mradi wa Ushirikiano kati ya Tanzania na Malawi wa mto Songwe.

§ Kuendeleza kilimo cha umwagiliaji Moshi Chini (Lower Moshi Integrated Agriculture & Rural Development Project) kwa msaada wa Serikali ya Japan.

**Maendeleo ya Ushirika**

58. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2000/2001 Wizara yangu itaendelea kuweka msisitizo katika ufungaji wa vitabu vya hesabu za Vyama vya Ushirika. Sambamba na hatua hii Wizara itaimarisha ukaguzi wa Vyama vya Ushirika ili ufanyike kwa wakati unaostahili na hivyo kusaidia kuzuia ubadhirifu wa mali za Vyama vya Ushirika.

59. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu itaendelea kuhamasisha wananchi kuanzisha Vyama vya Ushirika nchini kote ili waweze kuongeza tija, uzalishaji na ushindani katika ununuzi na uuzaji wa mazao. Aidha Wananchi hususan wanawake na vijana watahamasishwa kujiunga au kuanzisha Vyama vya Akiba na Mikopo (SACCOS) kama njia mojawapo ya kuwawezesha kuwa na mitaji. Vile vile Wizara itaendelea kutoa mafunzo kwa wanachama, wafanyakazi na watendaji wa Vyama vya Ushirika ili waweze kutekeleza vema majukumu yao.

**Marekebisho ya Mashirika ya Umma**

60. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu itaendelea kuzifanyia marekebisho sheria zinazohusu kilimo, mifugo na ushirika ili kuipatia sekta binafsi mazingira mazuri ya kushiriki katika maendeleo ya kilimo, mifugo na ushirika. Wizara yangu itaendelea kushirikiana na tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma (PSRC) katika zoezi la kubinafsisha mashirika ya umma ambayo bado hayajabinafsishwa. Aidha, Wizara itaendelea kurekebisha Bodi za mazao ili ziweze kukidhi majukumu ya kusimamia sheria na taratibu za mazao husika. Makampuni na mashirika yafuatayo yanategemewa kubinafsishwa katika kipindi cha 2000/2001:

- Shirika la Taifa la Usagishaji: Vinu vya mpunga vilivyoko Isaka, Tabora na Shinyanga. Vinu vya mahindi vilivyopo Iringa na Mtwara pamoja na vinu vya mahindi na ngano vilivyopo Arusha.

- Mashamba ya NAFCO; Mashamba ya mpunga ya Ruvu, Dakawa, Mbarali; Mradi wa Kapunga na mashamba ya mahindi Mbozi na Namtumbo.

- Mashamba ya Ngano ya Hanang: Basuto, Gawal, Gidaga Mowd Mulbadaw, Murjanda, Setchet na Warret.

- Karakana kubwa inayoshughulikia Mashamba yote ya ngano Hanang (Central Maintenance Service Centre – CMSC).

- Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) za Mkata, Dakawa, Kongwa na West Kilimanjaro.

- Kampuni ya Kusindika nyama cha Tanganyika Packers Limited – TPL.

- Mashamba ya Kampuni ya Chai; Mufindi, Maruku na tawi la Dabaga.

**Maendeleo ya Watumishi**

61. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2000/2001, Wizara yangu itaendelea kukamilisha kazi ya kuwaondolea watumishi kero zinazohusu utumishi wao. Wizara itafuatilia mara kwa mara mapendekezo yaliyopelekwa Tume ya Utumishi Serikalini ya kuwapandisha vyeo watumishi 7,243 waliopendekezwa kulingana na kibali cha Idara Kuu ya Utumishi. Pia itaendelea kurekebisha mishahara ya watumishi na kuwasilisha kwenye Halmashauri zinazohusika.

## III. SHUKRANI

62. Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii kuzishukuru Nchi na Mashirika mbalimbali ya Kimataifa ambayo yameisaidia sana Wizara yangu katika juhudi za kukiendeleza Kilimo, Mifugo na Ushirika. Kwanza napenda kuzishukuru nchi za Australia, Canada, China, Denmark, Finland, India, Ireland, Italia, Japan, Korea, Marekani, New Zealand, Norway, Ubelgiji, Ufaransa, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani, Uswisi na Sweden. Vile vile Mashirika na Taasisi za kimataifa kama ifuatavyo: Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, UNDP, FAO, EU, UNICEF, SADC, WFP, IFAD, CFC, CIMMIT, HPI, ICRAF, ICRISAT, IDRC, IITA na Sasakawa Global 2000. Bado tunahitaji misaada yao ili tuweze kuendeleza Kilimo, Ufugaji na Ushirika.

63. Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani za pekee kwa Wakulima na Wafugaji wa nchi hii kwa kazi kubwa wanayoifanya katika uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara katika mazingira magumu ya uhaba wa mvua na pembejeo. Aidha napenda kuwashukuru Waheshimiwa wabunge kwa michango yao ambayo imeiwezesha Wizara yangu kutekeleza mambo mengi kwa ufanisi mkubwa kwa nia ya kuwaendeleza wakulima na wafugaji nchini. Pia napenda kuwashukuru Manaibu Waziri, Mheshimiwa Profesa Pius Mbawala (Mb) na Mheshimiwa Ismail Iwvata (Mb), Katibu Mkuu wa Wizara, Ndugu Peter Barie pamoja na Wafanyakazi wote wa Wizara na Mashirika yote yaliyo chini ya Wizara yangu kwa kazi nzuri waliyoifanya licha ya hali ngumu waliyokumbana nayo katika kutekeleza majukumu ya Wizara. Mwisho natoa shukurani kwa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa kazi nzuri ya kuchapa hotuba hii.

## V. MAOMBI YA FEDHA 2000/2001.

64. Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe shilingi milioni 10,163.40 kwa ajili ya matumizi ya kawaida, na shilingi milioni 24,556.00 kwa ajili ya shughuli za maendeleo. Kati ya fedha hizi za Maendeleo, shilingi milioni 2,271.00 ni fedha za hapa na shilingi milioni 22,285.00 ni za nje.

65. Mheshimiwa Spika, na Waheshimiwa Wabunge nawashukuru kwa kunisikiliza.

**66. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.**